Muhtasari wa Changamoto

Pata maelezo zaidi kuhusu ndoto, madhumuni na malengo ya Changamoto ya BridgeBuilder ya 2018.

BridgeBuilder huwekeza katika ujenzi wa madaraja mapya na ya kipekee kati ya watu, mashirika, masuala, na imani kati ya mikingamano ya amani, mafanikio, na sayari. Kwa kufanya hivyo, BridgeBuilder inalenga kukuza uhusiano wa maana, utangamano mkubwa wa kijamii, na mabadiliko endelevu yanayoongozwa na jamii.

Changamoto ya Ubunifu

Tunawezaje kuja pamoja ili kushughulikia changamoto za kimataifa katika mikingamano ya amani, mafanikio, na sayari kwa njia mpya tofauti kabisa?

Ulimwengu wetu, nchi zetu, na jamii zetu zinapitia changamoto kubwa: kuanzia mizozo ya kutofautiana hadi majanga ya asili. Masuala haya yanazidi mipaka na tamaduni mbalimbali, yanahitaji umakinifu na ushirikiano wetu wa pamoja na mawazo mema ili kuyashinda.

Jamii mbalimbali zinashughulikia changamoto hizi kwa njia ambazo zinaweza kunufaika kutoka kwa msaada na mahusiano zaidi na wengine. Changamoto hii ya uvumbuzi—inayotekelezwa kwa kushirikiana na Wakfu wa GHR— itaunga mkono mashirika yanayoshughulikia changamoto muhimu za kimataifa kati ya mikingamano ya amani, mafanikio na sayari kwa njia mpya tofauti sana. Tunawezaje kuunda na kuvumbua pamoja kwa manufaa ya kimataifa?

Tarehe Muhimu:

- *Awamu ya Dhana:* Mei 1 - Juni 4
- *Mapendekezo Yanayostahili:* Juni 4
- *Orodha ya Walioteuliwa Iliyotangazwa:* Juni 21
- *Awamu ya Maoni ya Wafadhiliwa:* Juni 22 - Julai 13
- *Awamu ya Maoni ya Wataalamu:* Julai 14 - Julai 27
- *Awamu ya Kuboresha:* Julai 28 - Agosti 15
- *Utathmini na Jitihada:* Agosti 16 - Septemba 30
- *Dhana Bora Zilizotangazwa:* Oktoba 2018

Hitaji la Kuunda Madaraja

Changamoto za kimataifa ni ngumu na changamani, na haziwezi kutatuliwa kwa kutengwa. Iwe unashughulikia kuboresha amani, kuhakikisha mafanikio, au kulinda sayari yetu, kuna haja ya kubuni na kuunda njia ambazo zinajumuisha mitazamo mbalimbali, kwa kufuata kasi ambayo jamii ya kimataifa inasonga nayo na kubadilika. Kwa hivyo, kuunda na kudumisha mahusiano kati ya watu na maeneo ya masuala ni muhimu. Katika Changamoto yote ya Uvumbuzi, tunarejelea hii kama kazi ya 'kuunganisha'.

Hitaji la Ushirikiano wa Maana

Aina tofauti ya suluhisho inahitaji njia mpya ya kufanya kazi, katika jamii lengwa na kati yetu wenyewe kwa wenyewe. Michoro inaweza kupanua na kuwezesha aje mali ya kindani, badala ya kuendeleza uwezo wa kutokuwa sawa? BridgeBuilders inashughulikia changamoto hizi ngumu na changamani kwa njia inayowalenga wanadamu na jamii, kwa kuwawezesha watumiaji kufanikiwa na kukua kwa njia endelevu.

Kanuni za Kushirikiisha za BridgeBuilder:

Ili kuelekeza kazi yako, tumeangazia Kanuni hizi tano, ambazo zinaangazia maono ya BridgeBuilder ya njia ya kushirikisha na michoro. Tunatumaini wewe na mashirika yako yatapata nafasi za kutumia hizi katika miradi yako na kushirikisha katika Changamoto:

- **Kutana na watu mahali walipo.** Kijiografia, kijamii, kitamaduni, na kivinginevyo.
- **Unda mahusiano.** Kuza mahusiano ya uaminifu, halali na ya usawa yenye heshima na huruma.
- **Sikiliza kwa makini.** Sikiliza kwa unyenyekevu na ushughulikie hadithi za watu kwa uadilifu na heshima.
- **Fanya kazi kwa pamoja.** Fanya kazi na washiriki na jamii ili kuwasaidia na kuwawezesha katika mchakato wa kuhusisha maisha mapya na uchangamfu (aidha katika mazingira au jamii) kwenye jamii zao.
- **Jibu.** Shughulikia na ujumuishe mafunzo mapya mahusiano yanapoendelea kuimarika, ufahamu zaidi ukifichuliwa, na hali za jamii au muktadha zikibadilika.

Hitaji la Michoro Mwafaka

Tunatafuta dhana ambazo zitashughulikia umuhimu wa tatizo tukiunda bado na jamii ili kubadilisha hali kabisa. Tunavutiwa na suluhisho zilizoundwa *si kwa* bali *na* jamii lengwa. Kanuni Zetu za Michoro za BridgeBuilder zitaelekeza mchakato wetu wa kuwachagua washindi wetu, na zinapaswa kutumika kama nyota ya Kaskazini unapokuwa ukiunda suluhisho.

Kanuni za Michoro ya BridgeBuilder:

- **Shughulikia Mahitaji Muhimu.** Tunatafuta dhana ambazo zinashughulikia changamoto za haraka, muhimu za kimataifa na za kindani ambazo watu na jamii zinakumbana nazo katika mikingamano ya amani, mafanikio na sayari duniani. Dhana zitakazoshinda zitaonyesha vizuri hitaji muhimu ambalo dhana zao zinalenga kushughulikia.

- **Tumia Dhana katika Jamii.** Tunatafuta dhana ambazo zinatumia njia zinazotokana na muktadha, tamaduni, ufahamu, hekima, mahitaji, na maazimio ya jamii lengwa.

- **Kuza Njia Zinazolenga Usawa na Mifumo ya Haki Zaidi.** Tunatafuta dhana ambazo zina uwezo wa mabadiliko ya kudumu kwa kubadilisha miundo ya nguvu, kubadilisha hadithi, na kusogeza ulimwengu katika mwelekeo wa usawa na haki zaidi. Kwa maneno mengine, dhana ambazo zinawezesha Jamii, kuangazia uzuri, na kuwainua watu kufikia uwezo wao kamili.

- **Fuata Kanuni.** Tunatafuta dhana ambazo hutumia kanuni za Ushirikishaji na Michoro ya BridgeBuilder ili kuongoza mawazo, uamuzi, na hatua katika changamoto ya ugumu na kutokuwa na uhakika.

Maelekezo ya Uwasilishaji na Kigezo cha Utathmini

Uwasilishaji unakaribishwa kutoka kwa mashirika yasio ya faida, asasi za kiraia, jamii na ya faida yanayofanya kazi mahali popote nchini Marekani au duniani kote.

Maelekezo Yetu ya Uwasilishaji:

- **Unganisha maeneo mawili au zaidi ya mada:** Lazima dhana hizi zishughulikie maeneo mawili au zaidi ya mada (amani, mafanikio, na sayari).
- **Uasili:** Dhana hizi zinapaswa kulenga kuunda makabiliano ya kipekee kati ya watu, masuala, na Imani ambazo zinakuza mahusiano ya maana, utangamano mkubwa wa kijamii, na mabadiliko endelevu ya kijamii.
- **Inayoweza kuchukuliwa hatua na kuonekana:** Lazima dhana hizi ziweze kuchukuliwa hatua na kuwa na matokeo ya yanayoonekana katika jamii lengwa (badala ya utafiti, mikutano, ukuzaji sera, au utetezi).
- **Inayoweza kufadhiliwa:** Dhana ambazo zinaweza kutekelezwa ndani ya muda wa miezi 36 na maombi ya bajeti ya chini ya US$500,000.

Ng'amua zaidi kuhusu Kigezo chetu cha Utathmini na maelekezo na mahitaji ya uwasilishaji hapa.

Zawadi

Dhana bora zilizochaguliwa:

- Watapokea mgao wa $ milioni 1 katika ufadhili kutoka kwa Wakfu wa GHR
- Watajiunga na kundi la BridgeBuilder la mashirika bunifu yanayofanya kazi ili kushughulikia mahitaji muhimu
- Watashiriki katika wakfu wa kick-off , ambapo watakutana na wabunifu wengine wa kijamii na kuchora na kuunda zaidi njia zao na zana na utaalamu kutoka kwa Wakfu wa GHR na OpenIDEO
- Watapokea usaidizi unaoendelea wa ushirikiano kutoka kwa Wakfu wa GHR, mahusiano na mitandao ya wafadhili wengine, na kuonekana kwenye vyombo vya habari.

Je, Unafaa wapi?

Ikiwa shirika lako linafanya kazi ya kuunganisha tayari, tungependa kujifunza zaidi kuhusu jinsi Changamoto hii inaweza kuimarisha mradi wako. Ikiwa shirika lako linalenga jamii moja pekee au eneo moja la mada, jiunge na Changamoto letu la kuchunguza modeli mpya, kupanua uwezo wa kazi yako, na kuunganika na wengine wanaofanya kazi ambayo inaweza kulingana na misheni yako.

Je, bado una maswali kuhusu Changamoto hii? Hapa kuna baadhi ya mifano ya dhana bora kutoka kwa Changamoto ya 2017 ambayo tunatumaini itakuhimiza kushiriki au kujiunga na jamii hii:

Suluhisho linalounganisha Amani, Mafanikio na Sayari:
PeaceDirect: Inaunga mkono mashirika madogo ya kuchimbua dhahabu ya watu walioathiriwa na vita ili kuzalisha dhahabu inayofaa mazingira na ya kimaadili zaidi.

Suluhisho linalounganisha Sayari na Mafanikio:
Uhandisi wa BioKaboni (BioCarbon Engineering): Kuokoa maisha na kukabiliana na mabadiliko ya hali ya anga kwa kupanda miti haraka katika misitu ya jamii iliyoathirika ya pwani katika Myanmar kwa kutumia droni.

Suluhisho linalounganisha Mafanikio na Amani:
Kona ya Vijana wa Kameruni: Hukuza juhudi za ubunifu ili kuzuia/kukabiliana na magaidi kupitia kukuza uwezo/ujuzi wa ubunifu wa vijana wakosaji.

Mchakato wa Changamoto ya OpenIDEO

Wakati wa **Awamu ya Dhana,** tutatoa mwito kwa jamii yetu ya kimataifa kushiriki dhana ambazo zinawaleta watu pamoja ili kushughulikia changamoto muhimu katika mikingamano ya amani, mafanikio na sayari kwa njia mpya tofauti kabisa. Dhana hizi si lazima ziwe kamili au zimefanikishwa kabisa- kwa kweli, tunahimiza uwasilishaji wa mapema katika Awamu ya dhana ili Kushiriki kwa jamii kukuwezeshe kusisitiza na kuboresha dhana yako.

Kwa msaada kutoka kwa mdhamini wetu wa Changamoto, tutachagua dhana zilizowasilishwa ambazo zitaendelea hadi **Awamu ya Maoni ya Wafadhiliwa.** Wakati wa Awamu ya Maoni ya Mfadhiliwa, tutawaomba wachangiaji kujaribu dhana katika jamii zao na kutumia maoni katika mapendekezo yao. Washiriki waliochaguliwa watatarajiwa kushiriki kikamilifu katika kukusanya majibu ya watumiaji katika kiwango cha jamii. Unaweza kujifunza zaidi kuhusu yaliyomo katika mchakato hapo.

Wakati wa **Awamu ya Maoni ya Wataalamu,** dhana zilizochaguliwa zitakuwa na nafsi ya kulinganishwa na wataalamu kutoka kwa nyanja mbalimbali ili kukusanya maoni na ujuzi wa ziada. Baada ya maoni ya wataalamu, tutafungua **Awamu ya kuboresha,** ambapo kila dhana ina wiki tatu za kutumia majibu ya wataalamu katika mapendekezo yao, kuyakamilisha na kuyawasilisha upya pamoja na bajeti ya mradi.

Baada ya awamu hizi, tutapitia njia ya mkato na mdhamini wetu wa Changamoto— seti ya suluhisho zinazowakilisha uvumbuzi ambao unaangazia vyema moyo wa BridgeBuilder. **Dhana Bora** zitapokea ufadhili na usaidizi wa baada ya changamoto kutoka kwa GHR, na hata pia nafasi zinazoendelea za mahusiano na BridgeBuilders na OpenIDEO wengine.

Kuhusu Mdhamini wetu

Mdhamini wa Changamoto, GHR Foundation, anaongozwa na imani katika uwajibikaji, hatua, na ufahamu kwamba tumeunganishwa zote haijalishi umbari, dini, utaifa, au hali ya kiuchumi. Kwa zaidi ya miaka 50 na zaidi, GHR imekuwa ikiongoza katika kuunda muundo wa ufadhili inapokuwa ikishirikiana na wataalamu wa jamii ili kuunda na kuwezesha nafasi na mazingira mema ya kuwezesha mabadiliko. Wakfu huu unachukulia imani kama rasilimali muhimu ya wema—kiunganishi na kisawazishaji cha mabadiliko ya kijamii, na kiendeshi cha muunganisho kati ya watu, mitandao, masuala, na rasilimali. Iliyotiwa msukumo na imani ya Kikatoliki ya mwanzilishi, GHR inalenga kutumia Changamoto ya BridgeBuilder kuitikia mwito wa Papa Francis wa “kuunda madaraja” na kuchangia kufanya ulimwengu kuwa mahali pazuri kwa kuishi kwa binadamu wote.